# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

# BUNGE LA TANZANIA

## ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

## MKUTANO WA KUMI NA TISA

## KIKAO CHA ISHIRINI NA TANO

**15 MEI, 2025**

# ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

____________________

## MKUTANO WA KUMI NA TISA

## KIKAO CHA ISHIRINI NA TANO – TAREHE 15 MEI, 2025

**I. DUA:**

**II. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:**

**WAZIRI WA MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:**

Randama za Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026.

**WAZIRI WA UCHUKUZI:**

Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Uchukuzi kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026.

**MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MIUNDOMBINU:**

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu kuhusu Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara ya Uchukuzi kwa Mwaka wa Fedha

2024/2025 pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026.

## III. MASWALI:

### OFISI YA RAIS (TAMISEMI):

**319 MHESHIMIWA SHABANI OMARI SHEKILINDI (LUSHOTO):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, lini Serikali itapeleka Gari jipya la Wagonjwa katika Hospitali ya Wilaya ya Lushoto kwa kuwa gari lililopo limechakaa.

**320 MHESHIMIWA EMMANUEL ADAMSON MWAKASAKA (TABORA MJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, upi mkakati wa Serikali kukarabati Barabara za pembezoni Tabora Mjini.

**OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO NA MAZINGIRA):**

**321 MHESHIMIWA GEORGE NATANY MALIMA (MPWAPWA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira):-

Je, lini Serikali itaanza ujenzi wa kuimarisha kingo za korongo linalopita katikati ya Mji wa Mpwapwa ili kuzuia mmomonyoko na madhara kwa Wananchi.

**WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI:**

**322 MHESHIMIWA DKT. CHRISTINA CHRISTOPHER MNZAVA (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi:-

Je, nini mpango wa Serikali kuboresha Makazi ya Askari Polisi katika Manispaa ya Shinyanga kwa kuwa kwa sasa makazi hayo ni duni sana.

**WIZARA YA KILIMO:**

**323 MHESHIMIWA ENG. MWANAISHA NG'ANZI ULENGE (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo:-

Je, upi mkakati wa kuwaandaa Wanawake wakulima wa mbogamboga Mkoani Tanga kwenye mpango wa Tanga kuwa *Hub* ya Kilimo cha mbogamboga.

**324 MHESHIMIWA NAGHENJWA LIVINGSTONE KABOYOKA (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo:-

Je, lini ujenzi wa Bwawa la Yongoma - Same utaanza baada ya kukamilika kwa usanifu wa kina.

**WIZARA YA AFYA:**

**325 MHESHIMIWA DOROTHY GEORGE KILAVE (TEMEKE):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya:-

Je, kuna mpango gani wa kuongeza majengo katika Hospitali ya Rufaa ya Temeke.

**WIZARA YA MAJI:**

**326 MHESHIMIWA DANIEL AWACK TLEMAI (KARATU):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji:-

Je, lini Serikali itatimiza ahadi yake ya kupeleka Shilingi Bilioni 4.5 Karatu ili Wananchi wapate huduma ya uhakika ya maji.

## WIZARA YA UCHUKUZI:

**327 MHESHIMIWA MARGARET SIMWANZA SITTA (URAMBO):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Uchukuzi:-

Je, lini Uwanja wa Ndege Urambo utawekwa uzio kuimarisha usalama.

## WIZARA YA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WANAWAKE NA MAKUNDI MAALUM:

**328 MHESHIMIWA ASHA ABDULLAH JUMA (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum:-

Je, lini Serikali itaanzisha utaratibu wa kuwasajili Waendesha Bodaboda nchini.

## WIZARA YA UJENZI:

**329 MHESHIMIWA RASHID ABDALLAH SHANGAZI (MLALO):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi:-

Je, lini Serikali itajenga upya Barabara ya Mombo hadi Lushoto yenye Km 36 kwa kiwango cha lami ili kukidhi mahitaji ya sasa.

## IV. HOJA ZA SERIKALI:

### WAZIRI WA UCHUKUZI:

Kwamba, Bunge sasa likubali kupokea na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Uchukuzi kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026.

**DODOMA**
**15 MEI, 2025**

**BARAKA I. LEONARD**
**KATIBU WA BUNGE**